

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS TAMISEMI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KONDOA**

SHULE YA SEKONDARI BERABERA,  
S.L.P 217

**KONDOA**

**Tarehe.....**

**KUMB. NA: BSS/S3440/VOLI/ADM/0006**

MZAZI/MLEZI WA .....

**YAH:MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA**  
**SEKONDARI BERABERA MWAKA 2021**

**1:0 UTANGULIZI:**

- a) Uongozi wa shule ya Sekondari **BERABERA**, unafuraha kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza (I) mwaka 2021
- b) Shule itafunguliwa rasmi tarehe **11/01/2021**. Unatakiwa kuripoti saa **2:00 asubuhi**, fika bila kukosa .
- c) Kabla hujafika shuleni unatakiwa kupimwa afya yako katika hospitali ya serikali au kituo cha afya cha serikali na fomu iliyo ambatanishwa itajazwa na daktari anayetambulika na serikali.
- d) sheria zote za shule zinapaswa kufuatwa kikamilifu. Aidha fomu za sheria hizo zimeambatanishwa pamoja na barua hii.

**1:1 MAHITAJI**

**1:1.1 SARE ZA SHULE KWA WASICHANA**

- (i) Sketi mbili (2) za rangi ya kijani za marinda mapana yasiyozidi 10 na yasiyopungua 8 inayovuka magoti, (kitambaa kizito).
- (ii) Atakayevaa hijabu ashone kufuatana na utaratibu wa hijabu.
- (iii) Mashati mawili meupe, mikono mifupi, mfuko mmoja na yasiyo na marembo.
- (iv) Soksi nyeupe pea mbili.
- (v) Viatu vyeusi vya kufunika miguu vyenye kisigino kifupi na sio viatu vya plastiki (bajaji).
- (vi) Sweta rangi ya kijani yenye **V** mbele na **duara** nyuma .
- (vii) Unaruhusiwa kusuka (msuko wa mistari ya kwenda nyuma isiyopungua 5 na isiyozidi 7).

**1.1.2: SARE ZA SHULE KWA WAVULANA**

- a) Suruali mbili (2) rangi ya kijani yenye marinda mawili ya kuelekea nyuma na iwe pana.
- b) Mashati mawili (2) rangi nyeupe yenye mikono mifupi.
- c) Soksi pea mbili (2) ranginyeusi.
- d) Viatu vyeusi vya kufunika miguu vyenye kisigino kifupi pea mbili (2).
- e) Sweta la rangi ya kijani yenye shingo ya **V** mbele na **duara** kwa nyuma.
- f) Mkanda mweusi.

### **2.1.3 SARE ZA MICHEZO KWA WOTE**

- a) Bukta 1 rangi ya bluu/ Trakisuti.
- b) Raba pea 1 nyeusi.
- c) Tisheti 1 rangi ya bluu.
- d) Soksi nyeusi pea 1.

### **2:1:4 VIFAA VYA DARASANI**

- a) Madaftari makubwa yasiyopungua 10 na rula 1 ndefu ya sm 30.
- b) Mathematical set 1 kalamu za bluu au nyeusi zisizopungua 2 na penseli ndefu 1.
- c) Begi dogo kwa ajili ya kubebea vifaa vya darasani lisilo na picha (Rambo hairuhusiwi kabisa).

### **2:1:5. VIFAA VYA USAFI.**

Kila mwanafunzi awe na vifaa vyake vya usafi vifuatavyo:

  Kwanja,

  Jembe

  Ndoo na fagio la chelewa.

**ELIMU BORA KWA MAARIFA ENDELEVU**

.....

**MKUU WA SHULE**

#### **4:0: SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE .**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yamefafanuliwa kwa maandishi. Na utapewa nakala yako mara baada ya kuripoti shuleni.

- a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
- c. Kuwahi katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
- d. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
- e. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- f. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

#### **4:1 MAKOSA YAFUATAYO YAWENZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE .**

1. Wizi.
2. Uasherati na Ushoga.
3. Ubakaji.
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, sigara n.k.
5. Kupigana au kupiga.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
7. Kudharau Bendera ya taifa.
8. Kuo au kuolewa.
9. Kupata mimba au kuharibu mimba na nje ya shule.
10. Kutoa mimba.
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule.
12. kukataa adhabu kwa makusudi.
13. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.
14. Kukosa kufika shuleni kwa siku 90 mfululizo bila Taarifa rasmi.

#### **5:0: MAMBO MENGINE MUHIMU.**

- a. Medical Examination Form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
- b. Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi / Mkatiba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- c. Fomu ya Mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa Ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA BERABERA SEKONDARI.**

.....  
**MKUU WA SHULE.**

# KIAPO CHA MWANAFUNZI

PICHA

## KIAMBATANISHO A:

Mimi .....Mwanafunzi wa kidato cha kwanza (I) nimesoma na kuzielewa sheria za shule ya Sekondari **BERABERA**. Naahidi kuwa nitazitekeleza kadri ya uwezo wangu. Nikishindwa kuzitekeleza, hatua zichukuliwe na uongozi wa shule kulingana na kosa dhidi yangu. Hii ni pamoja na kusimamishwa au kufukuzwa shule.

.....  
Sahihi ya mwanafunzi

.....  
tarehe .....

Mtendaji wa Kijiji/ kata

Saini na Mhuri:.....Simu:.....

# KIAPO CHA MZAZI

## KIAMBATANISHO B : (MWANAFUNZI WA KUTWA)

Mimi ..... Mzazi/ mlezi nimekubali mtoto wangu.....Asume katika shule ya sekondari **BERABERA** tangu tarehe.....

- Ninaahidi kumpatia vifaa vilivyotajwa katika orodha na kuwa nitamhimiza mtoto wangu afanye bidii na kutii sheria zote za shule.
- Naelewa ya kuwa nafasi hii ya mtoto wangu kuingia kidato cha kwanza (I) siyo haki yake ila ni bahati aliyotunukiwa na Taifa.
- Naahidi ya kuwa nitahakikisha atafuata sheria za shule na ashindwapo hatua zozote zichukuliwe dhidi yake.

.....  
1.Jina la mzazi/ mlezi

.....  
tarehe .....

Namba ya simu: .....  
(Unaruhusiwa kuweka namba zaidi ya moja)

Tarehe..... saini & muhuri.....

2. Mwenyekiti wa mtaa / mtendaji.

Jina ..... Namba ya simu .....

# MEDICAL EXAMINATION FORM.

To be completed by a Medical Officer in respect of all I-IV entrants.

Full name of student : .....

Age ..... Sex ..... Year .....

1. Medical illness:.....
2. Blood Count Test:.....
3. Urine analysis Test:.....
4. STD's Test:.....
5. T.B. Test:.....
6. Eye Test:.....
7. Ears:.....
8. Spleen:.....
9. Abdomen:.....
10. Blood pressure:.....
11. Sickle cell:.....
12. Peptic ulcer:.....
13. Pregnancy Test (for Girls):.....
14. Epilepsy:.....
15. Any disease not mentioned above:.....

## ADDITIONAL INFORMATION:

E.g.: Physical defects or impairment (s) infections, chronic of family diseases etc

.....  
.....  
.....  
.....

.....

Name stamp

Designation

Signature and official

.....

.....

Station

Date

**NOTE:** Medical officer, during the course of this examination, please attends the individual according to any diagnosed case.

**N.B:** Fomu hii irudishwe shuleni pamoja na fomu ya kiapo na fomu ya mapokezi mwanafunzi/ mzazi azilete siku ya kuripoti shuleni. Mwanafunzi yeyote hatapokelewa bila fomu hii inayoonesha afya yake kuonesha kuweza au kutoweza kuendelea na masomo ya sekondari.